## Mafunzo Ya Namna Ya Kuwahudumia Watoto Yatima Na Wanaoishi Katika Mazingira Hatarishi

*Mradi wa ushirikiano wa ustawi wa jamii kuhusu UKIMWI kwa ajili ya watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi.*

**Siku ya 4**

## Mchakato Wa Huduma Kwa Ajili Ya Watoto Yatima Na Wale Walio Katika Mazingira Hatarishi Walioathiriwa Na UKIMWI

1.Kuwafikia na kuwatambua
2.Kujenga mahusiano na watoto na familia
3.Tathmini ya Mahitaji na Uwezo uliopo

## Mchakato Wa Huduma Kwa Ajili Ya Watoto Yatima Na Wale Walio Katika Mazingira Hatarishi Walioathiriwa Na UKIMWI

4.Kutengeneza mpango wa huduma: Kuunda mitandao, kufanya utambuzi na kutoa rufaa kwenye vyanzo vingine vya huduma
5. Kutoa huduma na misaada mingine iliyo ndani ya uwezo wa taasisi yako
•Kuwasaidia watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi
•Kutoa huduma ya ushauri nasaha pamoja na familia zao
•Kubuni mifumo saidizi kwa ajili ya watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi na familia zao
6. Kuendeleza Kesi menejimenti, utetezi pamoja na ufuatiliaji

## Melengo

***Mwisho wa siku msaidizi ustawi wa jamii atakuwa na uwezo wa:***

•Kutafsiri maana ya tathmini katika muktadha wa kufanya kazi na watoto walio katika mazinigira hatarishi pamoja na familia zao
•Kuonyesha sababu na mchakato wa kufanya tathmini
•Elezea umuhimu wa dhana ya uwezo katika kufanya tathmini ya mtoto na familia
•Elezea sifa za tathmini nzuri
•Tumia fomu ya makadirio ya hali ya mtoto kutathmini mahitaji ya watoto walio katika mazingira hatarishi pamoja na familia zao
•Kuweka kumbukumbu ya vipengele muhimu vya tathmini

*Tathmini*

Dhana ya Tathmini Jumuishi, Mahitaji na Uwezo.

## Nani Ameshawahi Kufanya Tathmini?

- Mjadala
- Ni nini maana ya Tathmini?

## Maana Ya Tathmini.

- ***Ni mchakato wa:***
- Kukusanya
- Kuchambua
- Kuunganisha
- Taarifa mbalimbali kuhusu mtoto na/au hali ya familia.
- ***Kwa madhumuni ya:***
- Kuelewa vitu vinavyosababisha hiyo hali
- Kubaini mahitaji ya kupewa kipaumbele
- Kupanga mikakati ya utatuzi
- Kutoa huduma

## Hatua Za Kutathmini

- ***Panga Tathmini.***
  - Unahitaji taarifa gani?
  - Habari hizo utazipata wapi?
  - Njia gani ni nzuri ya kupata habari
- ***Kusanya taarifa***
  - Ongea na mtoto, wanafamilia, wengine
  - Pitia Kumbukumbu- shule, afya na zingine
  - Tazama muonekano, tabia, mazingira
  - Taarifa za kitaalamu au nyaraka zingine

## Hatua Za Kutathmini

- ***Chambua taarifa***

-Je ni mahitaji gani muhimu ya kushughulikiwa?
-Je kuna uwezo au sifa gani ambazo zinaweza kusaidia kutimiza mahitaji?

- ***Kuhusianisha taarifa***

-Mambo gani yapewe kipaumbele?
-Mchakato uweje?

## Mchakato Wa Kutathmini.

- Mambo makuu ya kulenga unapoanza kukutana na mtoto na familia yake.
- Kumbuka kwamba tathmini ni mchakato endelevu unaodumu kwa muda wote utakaofanya kazi na mtoto na familia.
  - Mahitaji mapya yanajitokeza
  - Hali inabadilika kuwa nzuri
  - Mabadiliko mengine
  - Gundua mabadiliko
  - Fahamu ni wakati gani huduma zinahitaji kubadilika au kusitishwa

## Sifa Za Tathmini Nzuri

- ***Tathmini hufanyika vizuri kwa kushirikiana na mtoto na familia.***
  - Wana habari nyingi kuhusu hali zao.
  - Maisha yao yataathiriwa na maamuzi yatakayofanyika
  - Lazima wafanyie kazi mabadiliko yoyote.

## Sifa Za Tathmini Nzuri

- ***Tathmini zina manufaa kama zimelenga katika kuboresha***
  - Kulenga katika matatizo au mahitaji tu, kunachanganya na kumfanya mhudumiwa KUKATA TAMAA.
  - KILA MTU ana uwezo fulani, vitu vinavyoweza kuwa msingi wa mabadiliko
  - Kulenga katika uwezo wa mtu ni msingi mzuri wa kutatua matatizo na kuleta MATUMAINI.

## Misingi Ya Dhana Ya Uwezo

•Watu wote wana uwezo ambao unaweza kutumika katika kuboresha maisha.
•Tambua na himiza watu kutumia uwezo wao katika kila hali hata kama mtoto au familia haijihisi kuwa nao.
•Mruhusu mtoto au mwana familia kufanya maamuzi ya kile anachotaka kifanyike kwa kadri ya uwezo wao.

## Misingi Ya Dhana Ya Uwezo

•Kutambua uwezo kunahitaji ushirikiano kati ya msaidizi ustawi na mtoto au/na familia
•Kwa kutilia mkazo uwezo wa wateja msaidizi ustawi anajiweka kwenye hali nzuri ya kutowahukumu wateja wake
•Kutambua na kuheshimu rasilimali, ustahimilivu na uwezo wa kukabiliana na mazingira magumu

## Sifa Za Tathmini Zinazofanikiwa

•Tathimini inafanikiwa zaidi pale ambapo inamtazama mtu kwa ujumla ndani ya mazingira yake
•Watu huathiri na huathiriwa na mazigira yao
•***Mazingira ya kijamii:***
•Kaya
•Ndugu
•Makundi rika/marafiki
•Shule, majirani na makundi ya dini
•Rasilimali zinazotolewa na asasi za kiraia (mashirika yasiyo ya kiserikali, mashirika ya kiserikali)
•Mambo yanayochangia mahitaji NA utatuzi wa matatizo yako kwenye jamii ambayo mtoto anaishi

## Ngazi Za Tathmini

•Tunapofikiria juu ya mahitaji ya mtoto tunapaswa kuangalia wale watu ambao mtoto ana mahusiano nao ya karibu zaidi
•Tuanze na wale watu wa karibu zaidi
•***Baada ya hapo tunaenda kwa ndugu na marafiki***
•Baada ya hapo tunaangalia jamii pana pamoja na mashirika

## Hatua Ya I: Kupanga Tathmini

•***Jiandae:***
•Hakikisha una vifaa vyote utakavyohitaji( fomu, kalamu, n.k)
•Jitambulishe kwa serikali ya kijiji, pata baraka za viongozi, wazazi au walezi wa mtoto
•Mtambue mtoto
•Panga kuwatembelea mtoto na familia
•Mara nyingi itakua nyumbani kwao mtoto
•Inaweza kuwa mahali pengine ndani ya jamii husika

## Kuanza Kuwatembelea

•Salimia, na jitambulishe
•Fanya mazungumzo yasiyo rasmi kwa kadri uwezavyo
•Hakikisha ya kwamba mtoto aliyepo ndiye uliyepanga kumtembelea
•Eleza sababu za kuwatembelea-kujua mtoto na familia inaendeleaje
•Eleza kwa mlezi kwa nini ni muhimu wewe kujua jinsi familia inavyoendelea- ili kuangalia jinsi unavyoweza kuwasaidia
•Pata ridhaa yao kufanya tathmini
•Onyesha nia ya kweli na kuijali familia na mtoto

## *Hatua Ya II: Kukusanya Taarifa*

## *Mfumo Wa Kiekolojia*




**Taarifa kuhusu:**
**A.Mtoto**
**B.Familia**
**C.Ndugu na marafiki**
**D.Jamii**

*Ngazi ya mtoto*

## Hatua Ya II: Taarifa Kuhusu Mtoto

•Ni taarifa au mambo gani tunahitaji kujua wakati tunafanya tathmini ya mahitaji na uwezo wa mtoto?

Bungua Bongo

## Maeneo Ya Tathmini

1. Makazi
2. Saikolojia
3. Elimu na Maarifa
4 Afya
5. Chakula na lishe
6. Uboreshaji wa Uchumi
7. Ulinzi

## 1. Makazi

Tunawezaje kujua ya kwamba mtoto analala mahali ambapo panatosha, pakavu, na salama?

Bungua Bongo

## 1. Makazi

**Viashiria moja wapo**

•Nyumba imejengwa na nini?
•Je hii nyumba inatosha?
•Je nyumba inaonekana kuwa salama?
•Je nyumba inamlinda mtoto dhidi ya mvua na baridi?
•Je nyumba inahitaji merekebisho?

| **Maswali kwa mtoto( Itategemea na umri)** | **Maswali kwa mwana familia** |
|---|---|
| • Unaishi wapi?<br>• Una mahali pa kulala na kula wakati wote?<br>• Unalala wapi?<br>• Je huwa unalala mahali pengine? | • Mtoto anaishi wapi?<br>• Je mtoto ana mahali pa kulala na kula wakati wote?<br>• Mtoto analala wapi?<br>• Je huwa anakaa sehemu nyingine au kulala nje ya hapa? |

## 2. Saikolojia: Hisia

Tunawezaje kujua ya kwamba mtoto ana furaha, karidhika na mwenye matumaini?

Bungua bongo

## 2. Saikolojia: Hisia

***Viashiria moja wapo:***
•Je mtoto anaonekana mwenye furaha na mchangamfu?
•Je unaona ishara zozote za huzuni, wasiwasi au kutotaka kujichanganya?

| **Maswali kwa mtoto( Itategemea na umri)** | **Maswali kwa mwanafamilia** |
|---|---|
| • Je unajisikia mwenye furaha au huzuni mara nyingi?<br>•Je unafikiri una maisha mazuri?<br>•Je una matatizo katika kuhimili hisia zako?<br>•Je huwa unakasirika mara kwa mara?<br>•Je unahisi maisha yako yana sababu ya kuishi | •Je mtoto huwa na furaha au huzuni mara nyingi?<br>•unhappy? Unawezaje kujua ya kwamba mtoto huyu ana huzuni au furaha?<br>•Je huzuni ya huyu mtoto inakupa hofu?<br>•Je una hofu ya kwamba huyu mtoto anaweza kujidhuru? |

## 2. Saikolojia: Tabia Na Mahusiano Kijamii

***Viashiria moja wapo:***
•Je mtoto anahusiana vipi na wanafamilia wengine?
•Je mtoto anahusianaje na wewe kama msaidizi ustawi?

| **Maswali kwa mtoto( Itategemea na umri)** | **Maswali kwa mwanafamilia** |
|---|---|
| •Je una mahusiano mazuri na wakubwa zako?<br>•Je unaadhibiwa ukifanya kosa?<br>•Je unapenda kucheza na watoto wengine?<br>•Je una marafiki? Nieleze kidogo kuhusu marafiki zako. | •Je mtoto ana tabia gani kwa watu wakubwa?<br>•Je mtoto huyu anahitaji kuadhibiwa mara kwa mara?<br>•Je mtoto anachanganyikaje na watoto wengine?<br>• Nieleze kidogo kuhusu marafiki zake wa karibu. |

## 3. Elimu Na Maarifa

Unawezaje kupima maendeleo ya mtoto kielimu na kujifunza stadi za maisha nyumbani, shuleni, mafunzo ya kazi, au kazi zingine zinazolingana na umri wake?

Bungua Bongo

## 3a. Elimu Na Maarifa: Elimu Na Stadi Za Maisha

**3a.** ***Mtoto anaendelea vizuri kielimu na kujifunza stadi za maisha nyumbani, shuleni, mafunzo ya kazi, au kazi zingine zinazolingana na umri wakeViashiria moja wapo***

•Kama yuko shuleni, chunguza anavyoitikia unapomuuliza kuhusu amekua wa ngapi darasani

•Ikiwa mtoto ana umri wa miaka 5 au chini ya hapo, chunguza maendeleo kimakuzi (k.m lugha, mwendo, kujifunza) na linganisha na uwezo wa mtoto wa umri huo (k.m kuzungumza, kutembea katika umri wa miaka miwili)

| Maswali kwa mtoto( Itategemea na umri) | Maswali kwa mwanafamilia |
|---|---|
| •Je unafanya vitu vipya na kujifunza kutokana navyo?<br>•Ni stadi gani unajifunza au ungependa kujifunza (uliza watoto wakubwa)<br>• Je unafanya kazi za nyumbani? Unaweza kunielezea kidgo? | •Je huyu mtoto anajifunza vitu vipya kama unavyotegemea mtoto wa umri wake aweze kufanya?<br>•Walimu wanasemaje kuhusu maendeleo yake shuleni?<br>•Mtoto anafanyaje kazi za nyumbani?<br>•Je mtoto anapiga hatua shuleni kama anavyopaswa? |

## 3b. Elimu Na Maarifa: Kazi Za Shule Na Kazi Zinazoendana Na Umri Wa Mtoto

**3b.** ***Mtoto ameandikishwa na anahudhuria shule, anafanya michezo au kazi inayolingana na umri wake Viashiria moja wapo***

•Ikiwezakana chunguza sare yake ya shule au vifaa vya shule na matumizi yake

•Kwa watoto wadogo ambao hawajaanza shule angalia kama anashiriki kwenye michezo au kazi yoyote na mwanafamilia

| Maswali kwa mtoto( Itategemea na umri) | Maswali kwa mwanafamilia |
|---|---|
| •Je unaenda shule? Uko darasa la ngapi?<br>•Niambie kidogo kuhusu shule yako au mafunzo unayohudhuria<br>•Je umeshawahi kushindwa kwenda shule?<br>•Je una kazi?Unaenda kazini mara ngapi? | •Je mtoto anaenda shule ya msingi au amemaliza?<br>•Nieleze kidogo kuhusu shule ya mtoto au mafunzo anayohudhuria<br>•Nani analipa ada na kununua sare za shule? (kama hajamaliza, je huyu mtoto anaenda shule kila mara?<br>•Je mtoto amekosa kwenda shule mara ngapi kutokana na sababu nyingine?<br>•Je anaenda kazini mara kwa mara? |

# 4. Afya

Je tunawezaje kujua ya kwamba mtoto ana afya nzuri kimwili?

Je tunawezaje kupata taarifa za muhimu juu ya afya ya mtoto?

Bungua Bongo

# 4a. Afya Ya Mwili

***4a. -Mtoto anakua mwenye afya nzuri kimwili Viashiria moja wapo***

•Je mtoto anaonyesha kuwa mchangamfu na mwenye afya kwa ujumla?

•Je mtoto anasema ya kwamba anajisikia vizuri? ok in the Je amekua akijiskia vizuri katika kipindi cha wiki moja iliyopita?

•Je kuna dalili zozote za ugonjwa,ajali au matatizo mengine ya kiafya?

| Maswali kwa mtoto(Itategemea na umri) | Maswali kwa mwanafamilia |
|---|---|
| • Je una matatizo yoyote ya kiafya ambayo unafikiri tunaweza kukusaidia nayo?<br>• Je huwa unakosa kwenda shule au kazini kutokana na kuumwa? | • Nieleze kuhusu afya ya huyu mtoto<br>• Mtoto aliugua na nini mara ya mwisho?<br>• Je huwa anakosa kwenda shule au kazini kutokana na kuumwa |

# 4b. Huduma Za Afya

***4b. – Huduma za kiafya -- Mtoto anaweza kuzifikia huduma za kiafya ikiwemo matibabu wakati wa ugonjwa Viashiria moja wapo***

•Angalia kadi ya chanjo ya mtoto

•Je kuna chandarua cha kuzuia mbu?

| **Maswali kwa mtoto(Itategemea na umri)** | **Maswali kwa mwanafamilia** |
|---|---|
| • Ni nini hutokea wakati unaumwa?<br>• Je umeumwa hivi karibuni?Ulivyoumwa ulienda kupata matibabu?<br>• Je unatumia dawa?Kama ndio, unazipataje? | • Je nini hutukea wakati huyu mtoto anaumwa?<br>• Huwa unapataje dawa akihitaji?<br>• Je mtoto amewahi kupata chanjo?(kwa watoto walio chini ya miaka 5)<br>• Kwa watoto wa umri wa kubalehe, je kuna mtu yoyote amezungumza naye kuhusu VVU na jinsi ya kujikinga? |

# 5. Chakula Na Lishe

Je tunawezaje kujua ya kwamba mtoto ana chakula cha kutosha wakati wote?

Je tunawezaje kujua ya kwamba mtoto anakua vizuri kulinganisha na watoto wengine walio na umri sawa?

Bungua Bongo

# 5. Chakula Na Lishe

***5a. Mtoto ana chakula cha kutosha kwa wakati wote. Viashiria moja wapo:***

•Chunguza mazingira ya nyumbani-ghala la kuhifadhia chakula, bustani, na mifugo

•Je jiko linaonyesha kama limetumika kuandaa chakula katika kipindi cha muda mfupi uliopita?

| **Maswali kwa mtoto(Itategemea na umri)** | **Maswali kwa mwanafamilia** |
|---|---|
| • Je una chakula cha kutosha?<br>• Nani anakupikia chakula?<br>• Huwa unafanya nini wakati hakuna chakula cha kutosha? | • Familia inakula nini?<br>• Ulikula au mtoto alikula nini jana?<br>• Je familia hii inapataje chakula?<br>• Niambie kuhusu wakati ambao hakuna chakula cha kutosha |

# 5b. Lishe Na Kukua

**5b. Mtoto anakua vizuri kulinganisha na watoto wengine wa umri sawa katika eneo lake. Viashiria moja wapo:**

Linganisha mtoto amekua kwa kiwango gani tofauti na watoto wengine kwenye hilo eneo wenye umri sawa na yeye

| **Maswali kwa mtoto(Itategemea na umri)** | **Maswali kwa mwanafamilia** |
|---|---|
| • Je unafikiri unakuwa mrefu zaidi au mwenye nguvu zaidi ukijilinganisha na watoto wengine wa umri wako? | • Je ukuaji wa mtoto ukoje?<br>• Je anaonyesha kukua kama watoto wangine wenye umri sawa?<br>• Je una wasiwasi na ukuaji wa huyu mtoto?Uzito?Urefu? |

# 6. Uboreshaji Uchumi

Je tunawezaje kujua ya kwamba familia ina chanzo cha kipato cha kutosheleza na chenye kuaminika?

Bungua Bongo

# 6. Uboreshaji Uchumi

***6a. Familia ina chanzo cha kipato cha kuaminika na chenye kutosheleza.Viashiria moja wapo***

•Je nyumbani wana vitu, chakula na nguo kwa mtoto na wanafamilia wengine?

•Je una uhakika kwamba kuna fedha kidogo kuweza kukidhi mahitaji ya muhimu na dharura?

| Maswali kwa mtoto(Itategemea na umri) | Maswali kwa mwanafamilia |
|---|---|
| • Je wanaokulea wana pesa za kukununulia chakula na nguo?<br>• Je una pesa unazohitaji kwa ajili ya shule na mahitaji mengine?<br>• Je una kazi inayoweza kukusaidia kupata pesa unazohitaji?( kwa watoto wakubwa) | • Je unaisadiaje familia yako?<br>• Je kipato chako kinatoshelezaje mahitaji ya familia yako?<br>• Ni kwa kiwango gani kipato chako ni cha kuaminika?Je kuna kipindi katika mwaka ambapo huwa kinapungua/ongezeka?<br>• Je utalipaje gharama za matibabu ya mtoto ikihitajika? |

# 7. Ulinzi

Je unawezaje kujua iwapo mtoto hanyanyaswi, hajatelekwa au kutumikishwa

Je tunawezaje kujua iwapo mtoto anaweza kupata msaada wa kisheria ukihitajika?

Bungua Bongo

# 7. Ulinzi Na Utumikishaji Watoto

***7A. Mtoto hanyanyaswi, hajatelekezwa wala kutumikishwa.Viashiria moja wapo:***

•Je mtoto ana alama au michubuko yoyote ambayo inaweza ashiria unyanyasaji?

•Je mtoto anaonyesha dalili za kunyanyaswa, anajitenga au wenye hofu?

| Maswali kwa mtoto(Itategemea na umri) | Maswali kwa mwanafamilia |
|---|---|
| • Je unajihisi kuwa salama nyumbani na shuleni?<br>• Je unaweza kunieleza kuhusu wakati mtu alipokuumiza?<br>• Je unamfanyia mtu yoyote kazi nje ya nyumbani?<br>• Kama hujihisi kuwa salama unafikiri nani anaweza kusaidia? | • Je kuna mtu yoyote anamuumiza huyu mtoto?<br>• Je unahisi huyu mtoto anajisikia kuwa salama?<br>• Je mtoto anamfanyia kazi mtu yoyote nje ya nyumbani?<br>• Je kuna mtu mwingine yoyote anayemjua huyu mtoto ambaye anahisi kuwa mtoto huyu anaumiza? Au anadhalilishwa kingono? |

# 7. Msaada Wa Kisheria

**7b. Mtoto anaweza kupata huduma za msaada wa kisheria akihitaji. Viashiria moja wapo**

•Ikiwezekana, chunguza endapo mtoto ana hofu ya kupoteza mali za familia
•Je mlezi anaonyesha wasiwasi wowote au anasitasita akiulizwa kuhusu huduma za msaada wa kisheria kwa ajili ya mtoto?

| Maswali kwa mtoto(Itategemea na umri) | Maswali kwa mwanafamilia |
|---|---|
| • Je umewahi kuona cheti chako cha kuzaliwa?<br>• Je umeshawahi kujihisi ya kwamba haki zako hazieshimiwi<br>• Je mtu alishawahi kuchukua mali yako bila kukushirikisha?<br>• Je ulishwahi kulazimishwa kufanya kazi?<br>• Je kuna mtu mzima ambaye anaweza kukusaidia wakati wa mahitaji? | • Je mtoto ana cheti cha kuzaliwa?<br>• Je familia ina wosia?<br>• Je mtoto alishawahi kukosa/kunyimwa huduma yoyote kwa misingi ya sheria?<br>• Je una taarifa zozote za huyu mtoto kunyanyaswa kisheria kama vile kupokonywa ardhi?<br>• Je huyu mtoto ana mtu mzima wa kumsaidia kudai haki zake kisheria? |

## Mfumo Wa Kiekolojia




***Taarifa kuhusu:***
***A.Mtoto***
***B.Familia***
***C.Ndugu***
***D.Jamii***

*Ngazi ya mtoto*

# Hatua Ya II: Taarifa Za Familia/Kaya

***1.Nani anahusika na mtoto?***

•Taarifa za mtoto-Jina, umri/tarehe ya kuzaliwa, mahali anapoishi *( weka pia taarifa za mawasiliano)*
•Wazazi, ndugu. Majina yao, umri/tarehe ya kuzaliwa, mahali wanapoishi *(weka pia taarifa za mawasiliano)*
•Nani anaishi na mtoto kwa sasa?Jina, umri/tarehe ya kuzaliwa, uhusiano na mtoto *(weka majina ya watu wote wanaoishi kwenye kaya, pamoja na taarifa za mawasiliano)*
•Nani alikupa tarifa za mtoto au nani alimleta kwako kwa ajili ya kumsaidia? Jina, uhusiano na mtoto, na taarifa za mawasiliano za huyo mtu
•Watu wengine wanaohusika na mtoto. Jina, uhusiano na mtoto, wajibu wao kwa mtoto na taarifa za mawasiliano

# Taarifa Za Familia/Kaya

**3. *Tatizo ni nini?****(Tatizo linalofanya mtoto au familia iletwe kwako kwa msaada)*

•Kwa mtazamo wa yule anayemleta mtoto/familia
•Kwa mtazamo wa mtoto
•Kwa mtazamo wa wazazi
•Kama mlezi sio mzazi, pata pia mtazamo wake
•Mtazamo wa watu wengine wanaohusika na mtoto

## Mfumo Wa Kiekolojia




*Ngazi ya familia*

## Taarifa Kuhusu Marafiki Na Familia

***Je kuna mahitaji na rasilimali gani za kuweza kusaidia katika kutatua tatizo?***

- *Rasilimali binafsi na mikakati ya kifamilia kumudu hali (baini mahitaji, uwezo na mikakati ya kila mwanafamilia kukabiliana na hali): mtoto, watoto, wazazi, na wanafamilia wengine*
- Ndugu
- Marafiki

*Friends and Family level– improve this– add needs*

## Mfumo Wa Kiekolojia




*Ndugu na marafiki*

## Hatua Ya II: Taarifa Kuhusua Jamii

***Je kuna rasilimali gani na vyanzo vya msaada kuweza kusaidia katika kutatua tatizo?***

- Makundi ya kidini
- Asasi za kiraia
- Asasi za kiserikali
- Vyanzo vingine vya msaada/rasilimali

## Mfumo Wa Kiekolojia




*Marafiki na Jamii*

## Taarifa Nyingine: Historia Ya Tatizo

- ***Tatizo lilianzaje na lini?***
- ***Je tatizo limeendeleaje baada ya muda?***
- ***Ni vitu gani vingine ambavyo vinachochea na kushawishi tatizo***? (*Baini mahitaji na masuala yanayomsibu kila mwanafamilia: child(ren)Mtoto, watoto, Mzazi, Wazazi, na wengine )*

| | |
|---|---|
| •Mahitaji ya kiafya<br>•Mahitaji ya kisaikolojia<br>•Mahitaji ya kielimu<br>•Utumiaji madawa/kemikali<br>•Mahitaji ya kifedha<br>•Mabadiliko ya hivi karibuni | •Historia ya kupotelewa, kutengana<br>•Mtoto kudhalilishwa kimwili<br>•Mtoto kudhalilishwa kingono<br>•Kudhalilisha mwanandoa<br>•Mahitaji/vishawishi vingine |

## Jitihada Gani Zimechukuliwa Kujaribu Kutatua Tatizo?

•Mikakati gani imetumika kutatua tatizo?
•Huduma gani zimetolewa?
•Ni nini kimetokea baada ya kila jitihada?
•Kuna matunda yoyote?
•Changamoto?

## *Hatua Ya III: Chambua Taarifa*

Je tunawezaje kutumia taarifa tulizokusanya kujua masuala yanayohitaji kushughulikiwa na rasilimali zilizopo kuyashughulikia mahitaji?

## Uchambuzi Wa Taarifa

•Ni mahitaji gani yamebainika?
•How problematic are these needs? Je haya mahitaji yana uzito (madhara) kwa kiwango gani?
•Uwezo?
•Kw akuchunga kwa karibu, kuna mambo gani mengine ambayo unaweza kusema yanaendelea kwenye hii familia(ambayo hayajajitokeza)

## Dodoso La Makadirio Ya Hali Ya Mtoto

•Dodoso kwa ajili ya
•Kuchambua taarifa zitokanazo na tathmini
•Kuweka kumbukumbu ya tulichoona
•Kuanza kufikiria jinsi tuliyoyaona yanavyoweza kujumuishwa kwenye mpango wa kutatua tatizo

## Dodoso La Makadirio Ya Hali Ya Mtoto Kama Chombo Cha Kufanya Tathmini

•Liliandaliwa na kujaribiwa Ethiopia & Tanzania
•Chombo kinachomlenga mtoto
•Husaidia kubaini maeneo yenye mahitaji kulingana na hali ya mtoto
•Husaidia kufnaya tathmini ya mahitaji ya mtoto
•Linaweza kutumika kupima mabadiliko ya hali na mahitaji ya mtoto

## Dodoso La Makadirio Ya Hali Ya Mtoto Ni Nini?

•***Chombo cha kufanyia tathmini kinachotumiwa na Msaidizi Ustawi wa Jamii kujua***:
•Mazingira ya mahali mtoto anapoishi
•Mahitaji ya mtoto ya haraka
•Rasilimali ( Chakula, nyumba, mavazi) zinazohitajika kumsaidia mtoto haraka
•Huduma na watoa huduma wanaohitajika ili kumsaidia mtoto(elimu, afya,) sasa na baadaye

## Maeneo Ya Kutathmini

1. Malazi
2. Saikolojia
3. Elimu na Maarifa
4 Afya
5. Chakula na Lishe
6. Uboreshaji wa Kiuchumi
7. Ulinzi

## Dodoso La Makadirio Ya Hali Ya Mtoto



| Jina la mtathmini: | Jina la mtoto: | | Jina la mtoto: | | Jina la mtoto: | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jinsi: Me/Ke<br>Umri: | Uhusiano na mlezi: | Jinsi: Me/Ke<br>Umri: | Uhusiano na mlezi: | Jinsi: Me/Ke<br>Umri: | Uhusiano na mlezi: |
| | Tarehe | | Tarehe | | Tarehe | |
| II. AINA ZA HUDUMA | Alama (Zungushia moja) | Hatua ilyochukuliwa leo/msoni | Alama (Zungushia moja) | Hatua ilyochukuliwa leo/msoni | Alama (Zungushia moja) | Hatua ilyochukuliwa leo/msoni |
| 1. MAKAZI | | | | | | |
| 1a. Sehemu anayolala mtoto | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | |
| 2. SAIKOLOJIA | | | | | | |
| 2a. Hisia za hatiya | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | |
| 2b. tabia za kijamii | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | |
| 3. ELIMU NA MAARIFA | | | | | | |
| 3a. Uwezo wa utafiti | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | |
| 3b. Elimu/Kazi | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | |
| 4- AFYA | | | | | | |
| 4a. Ukamilifu kiafya | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | |
| 4b. Huduma za afya | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | |
| 5-CHAKULA NA LISHE | | | | | | |
| 5a. Ubaafka wa chakula | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | |
| 5b. Lishe na ukuaji | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | |
| 6-UBORESHAJI WA KIUCHUMI | | | | | | |
| 6a. Chanzo cha mapato | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | |
| 7. ULINZI | | | | | | |
| 7a. Unyanyasaji na utumikishaji | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | |
| 7b. Ufuatiliwa kisheria | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | | 4 3 2 1 | |
| Chanzo cha taarifa: (zungushia mayinuzika) | Mtoto, Mzazi/Mlezi, Ndugu, Jirani, Mwalimu, Rafiki wa familia, Mfanyakazi wa jamii, Wengineo | | Mtoto, Mzazi/Mlezi, Ndugu, Jirani, Mwalimu, Rafiki wa familia, Mfanyakazi wa jamii, Wengineo | | Mtoto, Mzazi/Mlezi, Ndugu, Jirani, Mwalimu, Rafiki wa familia, Mfanyakazi wa jamii, Wengineo | |



| ATUKO MUHIMU KATIKA KAYA: Weka alama kwenye kila kitu kinaa tangu alipotembelewa mara ya mwisho) | ___ Mtoto ameteka kwenye mpango<br>___ Mtoto amepata ujauzito<br>___ Mtoto amefariki<br>___ Mzazi kuugua<br>___ Mzazi/Mlezi amefariki<br>___ Mwanafamilia amefariki<br>___ Kubadilisha mlezi<br>___ Kuhama eneo la makazi<br>___ Unyanyasaji katika jamii (eleza ainа ya unyanyasaji)<br>___ Mengineyo (Taja)_____ | ___ Mtoto ameteka kwenye mpango<br>___ Mtoto amepata ujauzito<br>___ Mtoto amefariki<br>___ Mzazi kuugua<br>___ Mzazi/Mlezi amefariki<br>___ Mwanafamilia amefariki<br>___ Kubadilisha mlezi<br>___ Kuhama eneo la makazi<br>___ Unyanyasaji katika jamii (eleza ainа ya unyanyasaji)<br>___ Mengineyo (Taja)_____ | ___ Mtoto ameteka kwenye mpango<br>___ Mtoto amepata ujauzito<br>___ Mtoto amefariki<br>___ Mzazi kuugua<br>___ Mzazi/Mlezi amefariki<br>___ Mwanafamilia amefariki<br>___ Kubadilisha mlezi<br>___ Kuhama eneo la makazi<br>___ Unyanyasaji katika jamii (eleza ainа ya unyanyasaji)<br>___ Mengineyo (Taja)_____ |
|---|---|---|---|
| INA YA HUDUMA<br>ISTOLEWA (kwa kasi) | | Nani alitoa huduma? (mfano. Shinka lisilo la kiserikali, jirani, mwalimu, kanisa, n.k) | |
| duma ya chakula na fiaha (nsiheni ya chakula, chakula cha ba) | | | |
| kazi na huduma nyingine (ukarabati nyumba, malazi na e) | | | |
| ngaKuzimalezi (mlezi amepata mafunzo au mwaaba) | | | |
| zi dhidi ya unyanyasaji (Elimu dhidi ya unyanyasaji) toto au mlezi) | | | |
| aada wa kisheria (chati cha kuzaliwa, huduma za kisheria, o wa mirathi) | | | |
| ima za kafya (kama chanjo, matibabu, dawa za kupunguza ya ukimwi, kusamehewa ada ya huduma za afya, nyweleimu ya Ukimwi, rufaa) | | | |
| ada wa kisaikolojia (Kabu, kikundi, ushauri binafsi) | | | |
| ada ya kielimu (kusamehewa karo; kupewa sare za shule; ya shule, n.k) | | | |
| za maisha (elimu ya ukundi, fursa za kiuchu kwa familia) | | | |
| aidi zinazohitajika lau huduma zinazohitajika: | | | |

## Jinsi Ya kujaza Dodoso La Makadirio Ya Hali Ya Mtoto

•***Weka alama dhidi ya kila huduma kulingana na huu muongozo***

| | |
|---|---|
| **4 Nzuri** | Hakuna wasiwasi. Mahitaji yanatimizwa |
| **3 Wastani** | Kwa ujumla hali inakubalika lakini kuna wasiwasi kidogo kwa mujibu wa mlezi na mgeni |
| **2 Mbaya** | Hali ni tatizo kwa mtoto na familia |
| **1 Mbaya Zaidi** | Hali ni mbaya sana na inasabibisha matatizo makubwa kwa mtoto na familia |

## Mfano: Maana Ya Alama Za Dodoso– Chakula Na Lishe Kama Mfano(Rejea Jedwali Kwa Huduma Zingine)

***Nzuri na Wastani***

***NZURI = 4***
Mtoto anakua vizuri na urefu mzuri, uzito na nguvu kulingana na umri wake

***WASTANI = 3***
Mtoto anaonyesha kukua vizuri lakini sio mchangamfu sana kulinganisha na wengine walio na umri sawa

***Mbaya na Mbaya Zaidi***

***MBAYA = 2***
Mtoto ana uzito mdogo, na/au sio mchangamfu kulinganisha na watoto wengine wenye umri sawa

***MBAYA ZAIDI = 1***
(malnourished).Mtoto ana uzito mdogo sana (utapiamlo)na ni mfupi sana(kusinyaa) kulinganisha na umri wake

## Matukio Muhimu

•Dodoso lina sehemu ya kujaza matukio muhimu yaliyokea kwenye maisha ya mtoto
•Jaza matukio yoyote ambayo yametokea katika maisha ya mtoto tangu umtembelee mara ya mwisho( au katika kipindi cha mwaka mmoja kwa watoto ambao unawatembelea kwa mara ya kwanza)

## Kubaini Mahitaji Na Rasilimali: Mlezi Wa Familia

•Ni nini masuala au mahitaji ya msingi kwa mujibu wa mlezi au mzazi?
•Wazazi, walezi au ndugu wengine wa familia wana rasilimali gani?
• Je kuna masuala mengine mahususi yanayohusu wanafamilia wengine ambayo yanahitaji kushughulikiwa pia (ugonjwa wa mzazi, VVU, udhalilishaji wa kingono au kimwili, nk)?

## Kubaini Mahitaji Na Rasilimali: Ndugu Na Marafiki

•Ni ndugu au rafiki yupi anaisadia familia?
•Nani anasaidia wakati wa dharura au wakati pesa na rasilimali nyingine zinahitajika?
•Nani anamsaidia mzazi au mlezi?
•Je familia hii inalea ndugu wengine na hilo linamuathirije mtoto?

## Kubaini Mahitaji Na Rasilimali: Jamii

•Je kuna huduma gani ndani ya jamii?
•Je kuna mipango ambayo tayari inasaidia hii familia?
•Kama hakuna rasilimali, k.m huduma za afya, tunawezaje kufikia huduma zinazotolewa maeneo mengine?

## Huduma Au Rasilimali

• Sehemu nyingine ya Dodoso inatumika kuorodhesha aina ya huduma na rasilimali anazopatiwa mtoto, kaya, au taasisi wakati wa tathmini.
•Muulize mtu mzima kwenye maisha ya mtoto, mara nyingi itakua mzazi au mlezi, kuhusu hizi huduma na andika kwenye dodoso

*Hatua Ya IV: Kutimia Taarifa Kutengeneza Mpango*

Ni vipi vipaumbele vya huduma?
Mapendekeo: Ni hatua zipi zifuate

## Hatua Ya IV: Kutumia Taarifa Kwa Ajili Ya Kupanga

•Je ni yapi mahitaji ya muhimu zaidi yanayohitaji kufanyiwa kazi haraka? (orodesha kwenye fomu)
•Ni rasilimali gani ambazo zinaweza tumika?(orodhesha)
•Ungependekeza kuanzia wapi wakati tunatengeneza mpango wa huduma?
•Mapendekezo yako yanatengeneza msingi wa kuandaa mpango wa huduma kwa mtoto na familia (Tutajadili Mpango wa Huduma Siku ya 5)

## Mambo Ya Msingi Kuzingatia

•***Weka taarifa za familia siri (taarifa binafsi)***
- •Jaza dodoso kabla ya kuondoka kwenye eneo la familia
- •Taarifa hizi ni za familia. Andika kwa kifupi uliyoyapata ukiwa na familia kuhakikisha usahihi wa taarifa na kwamba wote wanakubaliana na hatua zifuatazo

## Mwongozo Wa Wakati Wa Ufuatiliaji

| Alama | Mwongozo wa kuweka alama | Mwongozo wa ufuatiliaji |
|---|---|---|
| 4 | Nzuri. | Hakuna haja ya ufuatiliaji. Unaweza kutoa taarifa za jumla juu ya upatikanaji wa huduma |
| 3 | Wastani | Itabidi kuchunguza hili eneo tena ukirudi kutembelea familia kuhakikisha ya kwamba hali haiendelei kuwa mbaya zaidi. Halionekani kuwa la dharura kwa sasa ila endapo msaidizi ustawi ana taarifa za kusaidia basi afahamishe wateja |
| 2 | Mbaya. | Inapendekezwa msaidizi ustawi asikilize ni nini mahitaji ya mtoto na familia na kama kuna huduma basi awaunganishe. Msaidizi anaweza kutoa rufaa moja kwa moja au akawasiliana na shirika husika au serikali ya kijiji isaidie familia |
| 1 | Mbaya zaidi | Ukiona kuna hali ya dharura kwa familia basi inatakiwa kutoa msaada haraka iwezekanavyo. Watakaotembelea hii familia wanatakiwa kutoa huduma moja kwa moja au kuwaunganisha na vyanzo vya huduma. Ikiwa hauna uhakika wa huduma ya haraka basi tengeneza mpango wa huduma kwa kushirikiana na mkuu wa shirika, mwenyekiti wa kijiji. Andika kila hatua utakayochukua kwenye dodoso |

## Kutumia Dodoso

•*Kumbuka Filamu ya Mwakaila*
•Fikiria tunawezaje kutathmini familia ya Mwakaila kwa kutumia dodoso la makadirio ya hali ya mtoto
•Tuangalie ni nini tunaweza kufanya ili kutathmini mahitaji na uwezo
- •Muulize mtoto au mwanafamilia
- •Chunguza nyumbani na kwenye jamii

•Gawanyikeni kwenye makundi 7-kila kikundi kichukue huduma mojawapo za kwenye dodoso

## Kutumia Dodoso

•Kila kikundi kitoe alama kwa familia ya Mwakaila kwenye eneo lao la huduma
•Tutajadili tulichojifunza kwa kutoa mrejesho mfupi

## Kazi Za Vikundi Kufanya Tathmini

•Kaeni kwenye makundi yenu manne
•Kwa kutumia kisa cha mmoja wenu kama mfano, igizeni Msaidizi Ustawi wa Jamii akifanya mahojiano na familia ili kufanya tathmini ya mahitaji ya mtoto
•Jaza tathmini yako kwenye dodoso kulingana na ulivyokadiria hali ya mtoto
•Jaza kwenye Dodoso la tathmini ya hali ya mtoto
•Jadilianeni mlichojifunza

## Rejea

•Nyangara, O'Donnell, Murphy & Nyberg (2009). Child Status Index A Tool for Assessing the Well-Being of Orphans and Vulnerable Children — Field Users' Guide. The Measurement Group.